



## **KIONGOZI WA SHULE YA SABATO**

### **KUHUSU MWONGOZO HUU**

Semina hii ya kiongozi wa Shule ya Sabato imejaa mambo tele yanayoweza kumsaidia kiongozi kuanza kazi au kuboresha kazi ya utumishi wake katika kanisa mahalia. Hapa kuna kazi na majukumu ya Kiongozi wa Shule ya Sabato, maelezo ya msingi yampasayo mtu ili kuanza kazi, vidokezo vya kuboresha kazi, jinsi ya kutafuta kutafuta maoni na kuipima huduma yako, na mengine mengi muhimu kwa ajili ya kazi ya Kiongozi wa Shule ya Sabato. Kwamba wewe ni mgeni wa kazi hii au ni mzoefu, mwongozo huu utakusaidia kupata mawazo mapya ambayo unaweza kuyatumia mara kadhaa katika kuboresha huduma za Shule ya Sabato kanisani kwako.

### **Mtaa wa Muheza**

Toleo la 1

## UTANGULIZI

Tangu wakati wa James White alipoanzisha kwa mara ya kwanza Shule ya Sabato ya Wanamarejeo kule Rochester, New York mnamo mwaka 1853, Shule ya Sabato imefanya kazi kubwa ktk makanisa mahalia. Utume wa Shule ya Sabato ni kuwafundisha watu jinsi ya kuipokea neema na kweli ya neno la Mungu na kumshirikisha kila mmoja ktk kuwaambia wengine juu ya mambo hayo. Shule ya Sabato si program ya Jumamosi asubuhi tu. Ni shule ya maisha ya Kikristo kwa ujumla.

Kulingana na utafiti ulifanywa kule North American Division na ofisi ya Habari na Utafiti, watu watatu kati ya wanne huja ktk shule ya sabato ili kutafuta kukuza maisha yao binafsi ya kiroho. Ili kufanikisha ukuaji huu, shule ya sabato inatakiwa kuwa na mipango makini iliyowekwa katika mfumo makini sana.

### Malengo makuu ya shule ya Sabato:

- 1) Kujifunza Biblia ambayo ni neno la Mungu (Kukaza maarifa)
- 2) Kudumisha ushirika na malezi ya wanashule ya sabato
- 3) Kuwa na mpango wa kuifikia jamii
- 4) Kuunga mkono utume wa kanisa

Kila kipengele kimoja katika malengo haya, ni cha muhimu sana, na kinaweza kufanikiwa ikiwa tutakua na mipango makini iliyowekwa vizuri

1. Kujifunza Biblia kunamsaidia mwanafunzi kuielewa injili na kufanya maamuzi ya kumfuata Kristo. Kujifunza Biblia pia humsaidia mtu kuishi maisha ya kiroho na humfundisha mtu kuzitafsiri kanuni za kimaandiko na kuishi maisha yake yeye mwenyewe kulingana na kanuni za maandiko.
2. Ushirika na Malezi huimarisha jamii ya wanashule ya sabato kwa kuinua viwango vya urafiki kupitia makundi madogo madogo ya shule ya sabato. Shule ya sabato, pia, ni njia ya msingi ya kufanya urejeshaji wa wale wanaoonekana kuchoka na safari.
3. Kuifikia jamii kunajumuisha jinsi ya kuwatia watu moyo kuwa na mbinu endelevu za uinjilisti. Kila darasa linatakiwa kuwa na mbinu za kufanya uinjilisti na mipango makini pia.
4. Kusisitiza utume wa kanisa la ulimwengu na njozi za Utume wa kanisa la Waadventista Wasabato. Shule ya sabato pia inakazi ya kuwasisitiza wanashule ya sabato kujitoa kikamilifu, na wakati mwingine kujinyima ili kuunga mkono utume wa kanisa ulimwenguni kote. Inakazi ya kuwajengea wanashule ya sabato hamu ya kuona hitaji la kusaidia ktk kukamilisha utume wa kanisa.

**Utafiti uneonyesha kwamba Shule ya Sabato haiwezi kufanikiwa vizuri isipokuwa kwanza imekua na program za uongoaji wa roho. "Shule ya Sabato inatakiwa kuwa moja kati ya vyombo vya muhimu sana, na vinavyofanya kazi, ya kuleta roho kwa Kristo." (Counsels on Sabbath School Work p. 10**

Je unatafuta jinsi ya kuboresha darasa lako la SS? Tembelea tovuti hii, japo yaliyopo hapo yako kwa lugha ya Kiingereza [www.nadadulthoodministries.org](http://www.nadadulthoodministries.org) Utakuta mambo ya

Shule ya sabato pamoja namiongozo ya Huduma Binafsi & Magerezani. Na mengine mengi kuihusu Shule ya Sabato.

## MAJUKUMU NA KAZI ZA MKUU WA SHULE YA SABATO

### Madarasa Ya Shule Ya Sabato Kama Familia Ndogo

"Historia ya shule ya sabato inatuonyesha wakati madara yalipokua yakikutana kujifunza neno, kuombeana, na kutoa fursa kwa kila mmoja kuzungumza changamoto zinazomkabili maishani na jinsi Bwana alivyowabariki. Madarasa yanatakiwa kuwa kama familia halisi au makundi ya kupeana uzoefu halisi wa maisha, Kwa hiyo kiongozi wa darasa ahakikishe kwamba wale wanaohudhuria madarasa yao wanakuza uhusiano wao na Mungu lakini na wanadarasa pia."

Kazi kubwa aliyonayo mkuu wa shule ya sabato, ambaye pia anajulikana kwa jina la Katibu wa shule ya sabato, ni kusimamia malengo makuu ya shule ya sabato. Wasaidizi wanaweza kuchaguliwa ili wafanye kazi na mkuu wa shule ya sabato.

Mkuu wa shule ya sabato ndiye mwenyekiti wa vikao vya shule ya sabato (Baraza la shule ya sabato), ambayo iko chini ya baraza la kanisa. Kupitisha mipango, program, miradi, na utekelezaji wa sera hutegemea sana utendaji wa baraza la shule ya sabato na uwajibikaji wake.

Wasaidizi wote wa vitengo mbalimbali, Viongozi wa madarasa, wanamuziki na mabawabu hutoa taarifa zao kwa katibu wa shule ya sabato/karani wa shule ya sabato.

Mkuu wa shule ya sabato hufanya kazi karibu sana na karani wa shule ya sabato, huku wakishirikiana na kamati/baraza la shule ya sabato katika kuchagua na kuwapatia mafunzo waalimu wa shule ya sabato, kuunda program bunifu, kusimamia fedha zinazotoka kwa bajeti ya kanisa kwa ajili ya shule ya sabato ili kukamilisha malengo yake manne.

Katika baadhi ya makanisa kunakua na wasaidizi kadhaa wanaoshirikiana na mkuu wa shule ya sabato ktk kukamilisha majukumu ya mkuu wa shule ya

sabato. Katika hali kama hiyo kuna njia mbili za kutekeleza majukumu ya uongozi huo:

1. Kila kiongozi anapewa program kadhaa za kusimamia kwa sabato kadhaa na anaweka mipango madhubuti ili kukamilisha mipango iliyowekwa. Au...
2. Kila kiongozi wa shule ya sabato anasimamia vitengo kadhaa vya shule ya sabato kwa mwaka mzima. Kwa mfano: mmoja anaweza kusimamia mambo ya utume wa shule ya sabato kwa mwaka mzima, wakati mwingine akishughulikia mambo ya ushirika na malezi ya wanashule wakati huo huo mwingine akisimamia jinsi watu wanavyojifunza neno (kukazia maarifa ya neno la Mungu) n.k.

## MAFUNZO MUHIMU YANAYOMFAA MTU KUWA KIONGOZI WA SHULE YA SABATO BORA

Hii inaweza kuwa kwa kiongozi wa shule ya sabato au huduma Binafsi, Imeandaliwa na Divisheni ya Kaskazini mwa Amerika, idara ya huduma Binafsi. Tumia mwongozo huu (mtaala huu) ili kuimarisha shughuli za Uanafunzi katika Shule ya sabato. Mafunzo muhimu ni pamoja na:

- Karama za Roho: Funguo ktk utume
- Kanuni za ushuhudiaji wa mtu Binafsi
- Kanuni za kiongozi mkristo
- Kanuni za Uongozi wa kikristo
- Jinsi ya kuelewa na kufundisha mafundi ya kanisa la waadventista wasabato
- Nguvu ya fursa: Ubatizo wa Roho Mtakatifu
- Kutengeneza na kutoa mafunzo ya mwalimu wa shule ya sabato
- Jinsi ya kujiandaa na kufundisha darasa la shule ya sabato
- Kuunda makundi madogo madogo ya shule ya sabato
- Jinsi ya kutafsiri Biblia na Roho ya Unabii
- Nguvu ya makundi madogo madogo
- Kanuni za uinjilisti katika maisha ya Yesu
- Mbinu za kutembelea nyumba kwa nyumba
- Kanuni na mbinu za kukatisha shauri
- Njia rahisi za kufanya mafundisho ya Biblia
- Uongoaji wa roho

### **Kusimamia vikao vya shule ya Sabato kama Mwenyekiti**

Kama mwenyekiti wa baraza la shule ya sabato, jambo la kwanza ni kujua mipango ya shule ya sabato kwa kusoma kitabu cha mwongozo wa shule ya sabato kinachoitwa *The Sabbath School Handbook*. Mara tu baada ya uchaguzi na hata baada ya uchaguzi, waite wanabaraza wa shule ya sabato pamoja ili kujadili uendeshwaji na maendeleo ya shule ya sabato. Baraza hili mara nyingi linaundwa na:

- Mkuu wa shule ya sabato
- Msaidizi wa mkuu wa shule ya sabato
- Karani wa shule ya sabato
- Wasaidizi wa karani wa shule ya sabato
- Wakuu wa vitengo mbalimbali vya shule ya sabato
- Mkuu wa uwekezaji
- Mkuu wa mambo ya utume
- Mkuu wa mfundisho ya Biblia wakati wa likizo
- Kiongozi wa shule ya sabato kundini
- Mchugaji au mzee wa kanisa kama mshauri

Kama mwenyekiti andaa ajenda za kila kikao, na uwaachie nafasi wakuu wa vitengo mbalimbali kuleta ajenda zao pia. Kila linalofanyika katika katika shule ya sabato linaamuliwa na baraza la shule ya sabato.

### **Kusimamia uchaguzi wa viongozi wa vikosi/madarasa ya shule ya sabato**

Ni jambo la muhimu sana kuchagua kwa makini wanaume na wanawake ambao watakua katika nafasi ya kutegemewa na viongozi wa shule ya sabato na kanisa pia katika kuiendesha shule hii makini sana. Unatakiwa ujue jambo flani kuhusu tabia yao na jinsi wanavyokua katika Kristo. Viongozi hawa wanatakiwa wawe na uwezo wa kumfikia kila mwanakikosi, binafsi. Wawe wema na waelewa, na waweze kuongoza mijadala ya mambo ya kiroho. “Wale ambao hufundisha madarasa ya shule ya sabato, wawe na mioyo yenye moto na wajazwe kwa kweli ya neno la Mungu, wasiwe tu wasikilazaji, bali pia watendaji wa neno. Waalimu wanapaswa kuwa wanafunzi makini wa neno la Mungu, na wadhihirishe kwamba kila siku wanajifunza masomo ktk shule ya Kristo, nao waweze pia kuwasilisha kwa wengine nuru waliyoipokea kutoka kwa Mwalimu mkuu Kristo, ambaye ni nuru ya ulimwengu.” (*Counsels on Sabbath School Work*, p. 93,94).

### **Shughuli za kiuongozi**

- Kupendekeza majina ya viongozi wa madarasa ya shule ya sabato (akisaidiwa na baraza la shule ya sabato)
- Kuhudhuria, na kuwatia moyo wengine kuhudhuria washa na mafunzo mbalimbali ya semina za uongozi
- Kutafuta miongozo ya kuwasaidia viongozi wa madarasa ya shule ya sabato
- Kuona kwamba kanisa linahitaji kuwa na miongozo mbalimbali (katika maktaba, ikiwa ipo) ya mbinu za kufundisha/kuongoza madarasa, jinsi ya kufanya program za shule ya sabato, ushuhudiaji, elimu ya utume ulimwenguni na miongozo ya kujifunza Biblia.

### **Kusimamia mipango ya shule ya sabato**

- Kuangalia kwamba mipango ya vitengo vya shule ya sabato vinakwenda sawa na kalenda ya kanisa.
- Kwa kushirikiana na kiongozi wa Huduma Binafsi, kuongoza kutekeleza mipango ya mwaka ya matukio ya kuifikia jamii kwa lengo la uinjilisti, mfano: kusimamia sabato za wageni, kusimamia huduma za uanzishaji na uendelezaji wa matawi ya shule ya sabato.
- Kuhakikisha kwamba mdarasa ya shule ya wabato yana idadi ya wanadarasa sita mpaka nane.
- Kuiwakilisha shule ya sabato na kuleta maombi ya mahitaji ya shule ya sabato kwa baraza la kanisa. Mfano vifaa au waalimu wa shule ya sabato. Kisha kuyaleta mapendekezo kwa baraza la kanisa kama kunahitaji hilo.

### **Kusimamia Program za kila juma**

- Kukazia sadaka tano za shule ya sabato: sadaka ya utume ya kila juma, sadaka ya kumi na tatu, sadaka za shukrani/kuzaliwa, sadaka ya uwekezaji na sadaka za uendeshaji wa shule ya sabato.
- Kupangilia kwa umakini wale watakaosimamia sabato ya kumi na tatu na kuiandaa
- Kwa kushirikiana na mchungaji, kuandaa darasa la mchungaji kwa ajili ya wageni wa imani na wale wanaopenda kujifunza zaidi
- Kuandaa/kusimamia program za shule ya sabato kila juma zinazowafanya na wanashule ya sabato kuwa na shauku ya kujifunza.

## Mawasiliano

- Kuwajulisha viongozi wenzake juu ya semina za konferensi matukio mengine kama washa zinazohusika na maeneo wanayotakiwa kufika, kukumbushia pia rale zinazokuja.
- Kutilia mkazo program mbalimbali za shule ya sabato ikiwa ni pamoja na utume kwa njia ya matangazo na njia zote za utangazaji.
- Kuyatembelea madarasa ya shule ya sabato mara kwa mara
- Kutafuta mbinu za kiubunifu za kutambua utendaji wa viongozi na madarasa yanayofanya vizuri katika shule ya sabato (appreciation)

## Kusimamia Siku Maalum za Program za Shule ya Sabato

Siku maalum ni njia muhimu kabisa katika uinjilisti kati ya njia muhimu, katika nyakati flani ndani ya mwaka. Kumbuka kuzifanya ziwe za kiinjilisti na chukua mawasiliano ili ufanye ufuatiliaji na yote haya yanatakiwa kuwa katika mpango kazi. Epuka kufanya program za siku maalum kama sabato ya wageni, bila kuwa na mbinu zozote zile za kiinjilisti.

Weka mkakati unaotekelezeka, wafanye watu kuwa wazalendo, weka program za kiroho, kumbuka kwamba lengo kubwa la siku maalum ni kumtengenezea mgeni hitaji la kutamani kuhudhuria tena kanisani wakati mwingine.

## Kusimamia Utunzaji wa Kumbukumbu

Kila darasa la shule ya sabato linatakiwa kuwa na orodha ya majina ya wanashule ya sabato inayoonyesha kumbukumbu muhimu za wanadarsa. Kiongozi wa darasa anayomamlaka ya kuongeza majina ya watu wanaotaka kujiunga ikiwa kuna nafasai na anpaswa kutoa taarifa haraka kwakarani wa shule ya sabato juu ya jambo hilo. Kumbukumbu hizi zinatakiwa kutazamwa mara kwa mara ili kuwatafuta wale ambao hawajafika kanisa kwa sabato kadhaa, au wale wenye taarifa zinazohitaji msaada wa wanadarasa.

Kumbukumbu hizi muhimu za wanashule ya sabato, zinatakiwa kuwa na mpango wa utume wa darasa (uinjilisti) na goli lake na kiwango kinachofikiwa ktk utekelezaji kwa kila juma. Taarifa ya shule ya sabato inatakiwa kutolewa kila juma ili kuonyesha jinsi shule ya sabato inayoendelea kimatoleo na kimahudhurio pia.

## Kutathimini Maendeleo ya Shule ya Sabato

Viongozi wa idara zinazofanikiwa mara zote huwa na nafasi ya kukaa na kufanya tathmini. Hufukiri juu ya mafanikio na mahali waliposhindwa kufikia lengo, na wanajifunza jambo flani kwa kila kitu. Wakiwa peke yao wanatafuta mashauri na kuwasikiliza wale wanaowakosoa kwa hekima na upendo au wale wanaotoa maoni.

Maswali kumi ya kujiuliza kama kiongozi wa shule ya sabato:

1. Je, taarifa za robo za shule ya sabato zimejazwa? Umeangalia na kugundua wapi kuna upengufu na kuushughulikia katika taarifa iliyojazwa?
2. Je ninaonyesha kumjali kila mwanashule ya sabato (katika kila kundi kati Tazama hadhira tano Uk. 9) na kumuhudumia kwa makini sana?
3. Je, ninawatia moyo waalimu na viongozi wa madarasa kutafuta jambo flani zuri (karama) ambalo analo mwanashule ya sabato katika kila darasa?
4. Je, ninawaambia viongozi wa madarasa kujifunza kutatua matatizo ya wanadarasa wao na wakati huo huo kuwafanya wawe huru kuja na kuzungumza nawe?
5. Je, ninaonyesha furaha na kumuamini kila kiongozi ninayefanya naye kazi ktk shule ya sabato?
6. Je, ninawashawishi watu wengine kuleta maoni na mawazo mapya ya uboreshaji wa shule ya sabato?
7. Je, ninafanya maamuzi kwa uangalifu, bila uonevu na haraka iwezekanavyo ili kutatua matatizo ya shule ya sabato?
8. Je, mimi ni mwainifu katika kutunza ahadi zangu na kusimamia majukumu ya shule ya sabato?
9. Je, ninakubali kwamba kunaweza kukawa na mabadiliko ya mbinu za kiutendaji na niko tayari kupokea mabadiliko hayo hata kama mimi si muasisi wa mawazo ya mabadiliko?
10. Je, ninajizuia kufanya matangazo marefu sana? Je, ninajizuia kutaka kuwatawla wengine kupita kiasi na kuwanyima uhuru?
11. Je, niko makini kuonyesha mfano bora kwa maneno, mwenendo na utekelezaji wa majukumu?
12. Je, Program za shule ya sabato zinauongoaji wa roho katika utendaji wake?

## **VIDOKEZO MUHIMU KWA KIONGOZI (*Mkuu wa shule ya sabato*)**

### **Kutenga muda kwa ajili ya Shule ya Sabato**

Takribani masaa 14 kwa mwezi ukiacha yale ya muda wa Siku za Sabato asubuhi, yanatakiwa kutengwa kwa ajili ya kazi hii. Mkuu wa shule ya sabato kwa upande wa watu wazima anatakiwa kutumia masaa mawili mpaka manne kwa mwezi katika kupangilia mambo ya shule ya sabato, kukusanya vitendea kazi na kuwasiliana na washiriki wa shule ya sabato. Angalau masaa mawili katika juma kando ya muda wa shule ya sabato (Jumamosi), yanatakiwa kutumika katika kupangilia na kuelekeza au kutoa mafunzo ya shule ya sabato. Lisaa limoja au mawili kwa mwezi hutakiwa kutumika kukutana na wanakamati wa shule ya sabato.

### **Wajibu wa kiongozi**

Wajibu wa mkuu wa shule ya sabato hugawanyika katika makundi makubwa manne:

- Kusimamia mambo ya kiuongozi
- Kusimamia mipango ya shule ya sabato
- Kusimamia program za kila juma
- Mawasilino

## MUUNDO WA PROGRAM YA SHULE YA SABATO

Shule nyingi za sabato hutumia sana mtindo wa kawaida unaofanana na huduma kuu. Huu hata hivyo si mpango ambao ni bora kabisa. Shule ya sabato inatakiwa kuwa na kushirikishwa na kujifunza kwa kila mtu. Tunayo Mashauri juu ya Shule ya Sabato na program zake:

“Lengo la shule ya sabato lisipotezwe ktk mipangilio yetu ya program, hivyo kupoteza muda ambao ungetumika kwa mambo mengine muhimu zaidi. Tunatakiwa kujilinda dhidi ya miundo na mitindo ambayo itatuondoa katika lengo tunalolifanyia kazi. Kunahatari ya kufanya mfumo wa shule ya sabato kuvuka mipaka (ktk program zake) na hivyo kuwa mzigo au *burudani zaidi*, wakati kiuhalisia inatakiwa kuwa mbaraka, yenye kufurahisha na kubariki. Kunamambo mengi sana yawewekwa katika muundo na namna ya kuiendesha (shule ya sabato), wakati uwezo wa Mungu unaoleta nguvu za kiroho haudhihiriki katika uongoaji wa roho, ambazo Kristo alizifia. **Mfumo wa mambo ni lazima ubadilishwe ikiwa shule ya sabato ipo kwa kusudi lililowekwa.**” (*Counsels on Sabbath School Work*, p. 151,156,157).

Mambo machache ya kuoboresha Shule yako ya Sabato:

- Weka mkakati wa Program zako kwa robo au mwezi
- Weka malengo ya mahudhurio, sadaka na miradi ya ss
- Yape madarasa majina mazuri na wajengee watu hali ya kuyapenda
- Kazia shule ya sabati ktk matangazo ya kanisa
- Kuwa na mafunzo mbalimbali
- Punguza muda wa program na ongeza muda wa madarasa kukaa pamoja.

Kadri tunavyotumia muda mwingi ktk kuwafanya wanashule ya sabato kuwa karibu katika makundi madogo madogo (madarasa), ndivyo watu wanavyojifunza zaidi na kutekeleza yale wanavyojifunza zaidi. Shule ya sabato ambazo humuacha mtu mmoja awe mzungumzaji mwanzo mpaka mwisho (Hata kama somo lake ni zuri kiasi gani) huwa na mguzo hafifu sana katika maisha ya mwanafunzi. Baraza la shule ya sabato chini ya mkuu wa shule ya sabato, huchagua mfumo wa program za shule ya sabato. Mfumo ufuatao waweza kutumika wakati wa kuanzisha shule, lakini kila shule yaweza kuweka mtindo na muundo wake kwa namna ya ubunifu wake.



**Muundo wa program ya shule ya sabato (Mfano 1)**

- 9:15 Ibada ya uimbaji (waalike watu tofauti kama watoto/vijana wasaidie kuongoza)
- 9:25 Maneno ya ukaribisho (ukaribisho, ombi)
- 9:30 Shule ya sabato na malengo yake makuu (chagua moja kwa kila juma)
- Msisitizo wa uinjilisti
  - Msisitizo wa kuifikia jamii
  - Msisitizo wa utume ulimwenguni kote
  - Uwekezaji
  - Maboresho (semina fupi za uboreshaji )
  - Taaraifa ya maendeleo (ifanye iwe zaidi ya kusoma namba)
  - Muda wa ushirika na maombi ya kuombeana
  - Jambo flani maalum la kuzungumzia/kufanya (chagua au panga jambo flani)
- 9:40 Muda wa madarasa ya shule ya sabato
- Shughuli za madarasa (dakika 125)
    - *Maombi*
    - *Changamoto za maisha*
    - *Uinjilisti na changamoto ktk uinjilisti*
    - *Mipango ya ushirika*
  - Kujifunza Biblia (lesoni) (dakika 30)
- 10:35 Matangazo ya mwisho, Maombi na kifuatacho juma lijalo (ikiwezekana)

**Muundo wa program ya shule ya sabato (Mfano 2)**

Muundo huu unatumia muda karibu sawa na muda unaotumika ktk muundo namba 1 hapo juu. (approximately 1.5 hours). Hata hivyo tofauti iko katika matumizi ya muda huo. Muundo huu huweka mkazo wake katika kuwaweka pamoja wanadarasa ili kujenga mazingira ya kujifunza zaidi na kutekeleza majukumu ya shule wakiwa kama darasa zaidi, hivyo kumpa kila mmoja muda wa kushiriki zaidi katika shughuli za shule ya sabato. Mfano wake ni huu ufuatao:

- 9:15 Mipango ya ushirika (kusalimiana, kushirikiana mawazo, maombi na uimbaji)
- 9:25 Shughuli za madarasa (watoto wanaenda kwenye madarasa yao; watu wazima wanabaki wakishughulika na mambo (*issues*) yanayohusu maisha maisha yao)
- 9:40 Utume ulimwenguni kote
- 9:50 Semina za mafunzo flani (mambo ya huduma binafsi na malezi)
- 10:10 Kujifunza Biblia katika madarasa ya shule ya sabato
- 10:35 Kufunga na kujua nini kinakuja sabato ijayo

*Zingatia:* Mpangilio wa matukio unaweza kubadilika na madarasa yanaweza kuchagua kuongeza muda juu ya jambo flani au kupunguza muda juu ya jambo flani.

## HADHIRA TANO ZA SHULE YA SABATO (Makundi 5 ktk shule ya sabato)

Utafiti unaonyesha kwamba katika kila kutaniko la shule ya sabato, angalau kuna makundi matano ya watu wanaohudhuria. Kila jamii ya kundi flani lina mambo linayoyatafuta na kuyapendelea zaidi.

Haya makundi yanaweza kugawanywa katika madarasa ili kukidhi mahitaji yao. Matokeo yake itakua ni kuongezeka kwa mahudhurio ya shule ya sabato. Kulingana na nafasi inavyopatikana, ni vizuri kuwa madarasa ya watu wazima kulingana na makundi yafuatayo:

Makundi hayo ni:

- Watu wanaokuja kanisani kwa desturi
- Watu wanaopenda sana mambo ya ushirika (u-pamoja)
- Wanaopenda kujifunza Biblia kwa kina sana
- Makundi ya kijamii
- Watu wanaopenda mambo mbalimbali

Kuwa na shule ya sabato yenye makundi haya ni jambo linalohitaji muda ktk kupangilia. Kila kundi na darasa linahitaji uongozi wenye mwalimu, mkaribishaji na kiongozi wa maombi. Hao wanatakiwa kutegemezana sana katika karama zao na kukutana mara kwa mara ktk maombi, kupanga na kutathimini kwa ajili ya madarasa yao. Kila timu ya viongozi inatakiwa kuhakikisha yale malengo manne ya shule ya sabato yamefikwa vizuri.

Mfumo huu wa makundi haya matano ktk shule ya sabato utapelekea kuwepo kwa Madarasa ya Shule ya sabato ambayo hukutana wakati wote wa shule ya sabato. Kila darasa litakua na muundo wake binafsi wa program na mtindo wake.

Tunapotumia mtindo huu, muda pekee tutakapokutana kama wanashule wote wa shule ya sabato, itakua tu kwa ajili ya kupata taarifa ya yale ambayo Mungu anayafanya pamoja na kumsifu kwa nyimbo.

Kufanikiwa kwa mtindo huu hutegemea mambo 3:

- Nafasi iliyopo katika jengo
- Kiwango cha kujituma na kujitoa katika kupangilia na
- kusimamia jambo hili, Uboru wa timu ya viongozi katika kila darasa la shule ya Sabato

### Makundi ya Utendaji katika Shule ya Sabato

Ikiwa njia ya makundi matano hayatafanya kazi katika shule yako ya sabato, huenda makundi madogo ya utendaji yanaweza kufanikiwa. Makundi madogo haya, mara nyingi huwa na watu sita mpaka nane ambao wamepangilia muda wao wa kukutana kwa program za shule ya sabato, kujifunza Biblia utume wa kanisa. Makundi haya husaidia sana katika malezi ya waumini wa shule ya sabato kwa kuwa watu hujenga ukaribu zaidi na kusaidiana ikiwa wako wachache.

#### **Charles Betz with Jack Calkins.**

Madarsa imara yaliyojazwa na Roho huweka mkazo katika kujifunza Biblia, kuboresha ushirika wa jamii ya waumini na kuboresha njia za kukuza uanafunzi. Mtu wa muhimu sana ktika kufanikisha jambo hili ni mwalimu wa darasa la shule ya sabato.

Mwalimu awe na mbinu za ufundishaji na awatie moyo wanadarasa kujifunza zaidi.

Kila kundi linakua na mwanalimu na kiongozi wa kundi. Hawa wanatakiwa kuwa na roho ya upendo, kujali, wawe wanashule hai wenye nia ya kumtangaza Kristo. Wanatakiwa pia kuwa na mbinu, kujitoa na wawe tayari kushirikiana na mkuu wa huduma binafsi.

Makundi madogo huendeleza mafunzo ya shule ya sabato, kuangalia kwa makini kile walichojifunza kwa juma zima na jinsi kinavyoweza kuwekwa katika vitendo vya Mkristo. Kazi ya kiongozi ni kutoa mafunzo na mwongozo kwa wanakikundi kwa namna rahisi inayoeleweka. Mwalimu humtia moyo kila mwanakikosi/kundi kujisomea Biblia, kuunda muhtasari na kuuliza maswali ya jinsi unavyoweza kuwashuhudia wengine kwa kutenda kile ulichojifunza.

### **Mfano wa program fupi ya Kundi**

9:15	Nyimbo maalum
9:25	Ukaribisho na ombi
9:30	Waimbaji/muziki maalum
9:35	Taarifa ya utume ulimwenguni
9:45	Shughuli za uinjilisti za kikundi zinaanza – takribani kwa dak. 25 Kujifunza Biblia – takribani kwa dak. 35
10:45	Ombi la kufunga

### **Kundi la ziada la huduma kwa wahitaji**

Hii ni sehemu ya shule ya sabato ambayo hushughulika na kujali mahitaji ya wanashule ya sabato ambao kwa sababu zisizoweza kuzuilika hawawezi kuhudhuria mara kwa mara kanisani. Kundi hili linaweza kuwa la watu wazee sana, wagonjwa au walemavu, au watu wengine ambao ni vigumu kufika kanisaani, kwa mfano wanajeshi. Katika baadhi ya makanisa kiongozi wa kundi hili huchaguliwa, akiwa na msaidizi mmoja kwa kila kundi la watu kumi wanaohitaji kutembelewa. Ikiwa wanadara chini ya wanne wako katika darasa hili, kiongozi mmoja wapo wa shule ya sabato anapaswa awatembelea na kuwapatia miongozo ya kujifunzia Biblia na miongozo mingine inayoweza kuwasaidia ktk maisha yao ya kiroho.

### **Miongozo ya kujifunza Biblia (lesoni)**

Ni vizuri kuhakikisha kwamba kila darasa limepangwa kwa kuzingatia zile hadhira tano za shule ya sabato, lakini pia kwa kuzingatia mgawanyo wa umri ili kujifunza miongozo ya Biblia kwa umri stahiki unaoendana na mwongozo anaokuwa nao mwanashule ya sabato. Viongozi wa shule ya sabato wahakikishe kwamba kila mwanashule ya sabato amepata mwongozo wa kujifunza Biblia na anayo Biblia ili kufikia lengo la shule ya sabato la kujifunza na kukaza maarifa ya neno la Mungu.

### **Tawi la Shule ya Sabato**

Darasa moja au zaidi ktk shule yako ya sabato linaweza kuamua kuanzisha tawi la shule ya sabato mahali flani. Hili tawi la shule linaweza kukutana mahali popote mazingira yanaporuhusu na katika siku yoyote ile ya juma. Kwa maelezo zaidi juu ya tawi la shule ya sabato angalia mwongozo wa Shule ya Sabato.

## Maelezo ya Ziada kwa Mkuu wa Shule ya Sabato ya Shule ya Watu Wazima

Lengo kuu la shule ya sabato ni kuwafanya watu kuwa wanafunzi wa Kristo. Hii ni pamoja na malezi ya kiroho kwa wanashule na wale wanaotarajiwa kujiunga na shule hii, lakini pia hata kwa wale ambao hawana dhehebu lolote lile wanatafuta tu kujumuika katika jamii, kwa wale wanaopenda kujifunza neno la Mungu, na wale wanaopenda tu kushiriki baadhi ya program za shule na kutoa au kupokea huduma flani za shule hii. Shule ya sabato haipo tu kwa ajili ya wanashule waliopo ndani ya kanisa tu, lakini pia kuwafunza wanashule kuweza kuwahudumia wengine ambao wako nje ya shule. Shule ya sabato ni shule inayofundisha maisha ya Kikristo, sio tu matukio ya siku ya sabato asubuhi. Kusudi lake ni uinjilisti wala sio desturi za ibada.

Kila muumini ameitwa kwa ajili ya uinjilisti na utume, kila muumini amepewa jambo flani na Roho wa Mungu ili atumike. Na pia katika ubatizo tunapewa agizo la kwenda kutumika, Waefeso 4:11-12

*“na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake. Nasi katika huyo tupate kuwa sifa ya utukufu wake, sisi tuliutangulia kumwekea Kristo tumaini letu.”*

Matendo 2:42-47

*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali. Kila mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume. “Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika, wakiuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja. Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.”*

Biblia inatupatia msingi wa kile shule ya sabato inachotakiwa kufanya. Fungu la 42 linatupatia lengo la shule ya sabato ambalo ni “kufundisha na ushirika” na “kuumega mkate pamoja na maombi pia.” Mafungu ya 43-45 yanaonyesha mfano bora wa wahusiano ya umoja, kila mtu kumjali mwenzake na kuungana mkono (support) kunakotakiwa kuwepo katika shule ya sabato ili kuwa na mazingira mazuri katika kujifunza na kukua kiroho. Fungu la 46 linaonyesha hili linaweza kutokea ndani na nje ya jengo la kanisa, katika makundi ya kujifunza Biblia nyumbani au katika kile ambacho Waadventista wamekiita Tawi la shule ya sabato, na fungu la 47 linaonyesha jinsi kanisa linavyoweza kukua kwa kutumia njia hii.

Shule ya sabato inaendeshwa kwa kutegemea juhudi za kujitoa kwa mtu mmoja mmoja. Inaendeshwa, kusimamiwa na kupata ufadhili wa waumini wa kanisa. Mungu anamuita kila mwanashule ya sabato katika huduma za kanisa, na shule ya sabato ni sehemu ya maandalizi ya kumtayarisha mtu na kumuwezesha kutumika. Kwa hiyo basi ni jambo la muhimu kuwa na ufahamu wa wahusika katika shule ya sabato.

## KAZI ZA MKUU WA SHULE YA SABATO

Huduma ya mtu anayelitwa kuwa mkuu wa shule ya sabato, inaweza kuelezwa kama ifuatavyo:

1. *Mambo ya kiuongozi:* Utawasimamia viongozi wote wa shule ya sabato na kuwatia moyo kufanya na kufanyiwa tathimini za utendaji wa majukumu yao, madarasa ya shule ya sabato na shule ya sabato kwa ujumla katika kufikia malengo ya kanisa. Unatakiwa kuweka mipango ya kuwapatia mafunzo, kuwasaidia pale wanapohitaji msaada wa kiuongozi na miongozo na vitendea kazi.
2. *Kuwa mwenyekiti wa baraza la shule ya sabato.* Kundi hili linajumuisha mkuu wa shule ya sabato, wasaidizi wake, makarani, wasaidizi wa makarani, viongozi wa vitengo mbalimbali vya shule ya sabato, kiongozi wa uwekezaji, kiongozi wa waalimu wa shule ya sabato na mzee wa kanisa au mchungaji kama washauri.
3. *Kuunda mkakati bora wa uinjilisti.* Isaidie timu yako kujenga mazingira mazuri ya kujifunza, kila mmoja kumjali mwenzake na mafunzo yanayomkuza mtu kiimani.
4. *Kuandaa watu wanaojitolea.* Kuna hitaji la kudumu la kutafuta watu watakaokua watoaji wa msaada kwa shughuli mbalimbali za shule ya sabato. Wewe ndiwe unatakiwa kuchukua hatua za kuwafuata na kuwaalika peke yao ili wahusike, na kuwasaidia jinsi wanavyoweza kuanza kutoa msaada ili kuiungamkono shule ya sabato (kuwa mbunifu wa mambo wanavyoweza kufanya)
5. *Kuweka mkakati kazi.* Itakua ni jambo zuri kuwasaidia viongozi wenzako wa shule ya sabato kupangilia mambo ya baadae kabla ya baraza la kanisa au baraza la shule ya sabato.

**Kiongozi bora wa shule ya sabato atakumbuka mambo yafuatayo:**

Binafsi, ukue kiroho; toa na poka mawazo kwa wengine, kuwa mtu wa matumaini na mchapakazi mvumilivu, kusanya nuru ya mafunzo mbalimbali, tafuta nguvu na kuwatia moyo au kutiwa moyo na wengine, kuwa mtu wa maombi, uinjilisti na kuifikia jamii – hii ndiyo yote juu ya shule ya sabato.